**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA BALOZI DKT. EMMANUEL JOHN NCHIMBI, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KATIKA MKUTANO MKUU WA URATHI WA MKAPA (MKAPA LEGACY SUMMIT)

**DAR ES SALAAM**

**16 JULAI 2026**

**Kazi na utu...**

Kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninayofuraha kujumuika nanyi katika Mkutano huu muhimu unaoangazia maisha, kazi na mchango wa Kiongozi wa Taifa letu Hayati Benjamin William Mkapa. Mheshimiwa Rais alipenda kushiriki tukio hili lakini kutokana na mwingiliano wa majukumu ameshindwa na hivyo amenituma kumwakilisha. Hata hivyo, Mheshimiwa Rais amenituma niwahakikishie kuwa anathamini sana mchango wa Hayati Benjamin William Mkapa. Yeye binafsi, daima amejitahidi kufuata nyayo zake, kwa kuendeleza na kujenga juu ya msingi wa urithi aliouacha.

Nawaomba sasa tusimame kwa dakika moja ya ukimya ili kumkumbuka Hayati Rais Benjamin William Mkapa na kutafakari mchango wake mkubwa kwa Taifa letu, bara la Afrika na dunia nzima...Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi!

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Leo katika kongamano hili tunaadhimisha maisha yenye mafanikio ya Hayati Mkapa ikiwa ni miaka sita tangu kifo chake na miaka ishirini tangu kuanzishwa kwa Taasisi ya Benjamin Mkapa. Katika uhai wake, Hayati Mkapa aliamini katika kujenga taasisi na alitumia muda wake, nguvu na jitihada zake nyingi kuhakikisha taasisi hizo zinaimarika. Ushahidi upo unaoonesha kuwa taasisi nyingi zilizoasisiwa katika uongozi wake (ikiwemo hii ya Benjamin Mkapa Foundation) bado zinaendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Kama mnavyofahamu, Taasisi ya Benjamin Mkapa ilianza na jitihada za kusaidia Serikali katika mapambano dhidi ya UKIMWI, na baadaye ikaelekeza nguvu zake katika kuboresha upatikanaji wa huduma za afya katika maeneo ya pembezoni na yenye uhaba wa rasilimali kwa kujenga nyumba za watumishi wa afya ili kuwavutia na kuwahifadhi katika maeneo hayo. Vilevile, taasisi ikajikita katika ajenda ya Rasilimaliwatu katika Sekta ya Afya (*Human Resources for Health – HRH*), ambayo ilikuwa muhimu sana katika kukabiliana na changamoto za afya. Leo hii tunaiona taasisi ikiwa mstari wa mbele katika kuendeleza uimara wa mifumo ya afya na kuandaa kizazi kijacho cha wataalamu wa afya. Kwa njia hiyo, taasisi imeonesha uthabiti katika kutafuta suluhisho la changamoto mbalimbali, na hata kujitofautisha na taasisi

nyingine na kujifungamanisha na washirika wa kweli na wawezeshaji wa jitihada hizo.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Sote tulimfahamu Hayati Benjamin Mkapa kama kiongozi jasiri, mwenye maono na asiyekwepa changamoto bali aliyekabiliana nazo moja kwa moja. Kutokana na hilo, nimevutiwa na kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu isemayo: ***"Kutoka Urithi hadi Mustakabali: Uongozi, Mifumo ya Afya, na Mtaji Watu unaoongozwa na Vijana kwa Afrika."*** kwani inatuelekeza kuangalia mbele na kuelekea mustakabali ulio bora badala ya kutazama hapa tulipo. Pia, inatukumbusha kutambua kuwa afya njema ni muhimu kwa maendeleo, na umuhimu wake unaongezeka zaidi kwa kuangalia mchango wake katika kujenga rasilimaliwatu. Ili rasilimaliwatu iweze kuchangia kikamilifu maendeleo kiuchumi na kijamii, lazima iwe na afya njema, na iweze kuishi kwa muda mrefu *(longer life-expectancy)*. Hii inajumuisha kuhakikisha watoto wanapata lishe bora, chanjo muhimu na kinga dhidi ya magonjwa; vijana wanapata elimu sahihi ya afya ya uzazi na kujikinga na magonjwa ya kuambukiza; jamii nzima inakingwa dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza; na huduma stahiki kwa wazee.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Maisha na uongozi wa Hayati Benjamin Mkapa unatoa mafunzo mengi kwetu. Mathalan,katika usimamizi na uendelezaji wa sekta ya afya, tunajifunza:

**Kwanza**, kutambua nafasi ya afya bora katika maendeleo. Hili tunaliona tangu awamu ya kwanza ya uongozi wa Taifa letu, ambapo Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alitangaza maradhi kuwa miongoni mwa maadui watatu wa Taifa letu. Aidha, Hayati Benjamin Mkapa katika awamu yake aliweka mkazo katika mapambano dhidi ya UKIMWI (ambapo alianzisha TACAIDS kuongoza mapambano hayo), Malaria na magonjwa mengine yanayoambukizwa na yasiyo ya kuambukiza. Vilevile, viongozi wa awamu nyingine akiwemo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na wewe Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, mmeendeleza jitihada hizo kwa kusimama kidete kuongoza mapambano dhidi ya UVIKO-19 na magonjwa mengine.

**Pili**, tunajifunza kuwa sekta ya afya inahitaji viongozi walioandaliwa vizuri na kuwezeshwa kikamilifu. Uongozi wa afya ni taaluma yenye maarifa na ujuzi

wa kipekee unaojengwa kupitia mafunzo, uzoefu na malezi ya kitaaluma (*mentorship*). Ni muhimu kiongozi katika sekta ya afya kuelewa uhusiano uliopo kati ya afya na uchumi, siasa, utamaduni, pamoja na muunganiko kati ya mifumo ya afya ya kitaifa na ya kimataifa. Nafurahi kuona kwamba Taasisi ya Benjamin Mkapa imechangia kwa sehemu kubwa kuwezesha viongozi katika sekta ya afya.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Nichukue fursa hii kuipongeza kwa dhati Taasisi ya Benjamin Mkapa kwa kuwekeza katika maandalizi ya viongozi wa afya hususan kupitia programu yenye mafanikio ya ***Mkapa Fellows Program*** na sasa kupitia ***Mkapa Health Leadership Programme*** itakayozinduliwa hivi karibuni. Hili ni eneo muhimu ambalo kwa bahati mbaya halikupewa kipaumbele cha kutosha licha ya umuhimu wake, hususan katika kipindi hiki ambapo changamoto za kiafya duniani zimekuwa zikiongezeka, na maandalizi dhidi ya milipuko ya magonjwa yamekuwa hitaji la lazima. Hata hivyo tunahitaji kwenda mbali zaidi na kuimarisha mifumo ya afya iliyoratibiwa, yenye ufanisi na inayoweza kuzuia majanga kabla hayajatokea. Ninaipongeza Taasisi ya Benjamin Mkapa kwa kuwa mstari wa mbele katika kuongoza ajenda hii

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Tunapotafakari kuhusu mustakabali wa utoaji huduma za afya, hatuna budi kutoa kipaumbele kwa vijana kama Hayati Mkapa alivyoamini, kwani hakuna mustakabali mwema bila wao. Vijana ndiyo viongozi wa sekta ya afya wa kesho, watumishi wa afya na watafiti wajao. Kwa kuzingatia hilo, tunalazimika kubuni programu zitakazowaandaa vijana kukabiliana na changamoto za siku zijazo kwa kujiamini.

Kwa kutambua hilo, Serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuwekeza kwa kiwango kikubwa katika kukuza elimu ya sayansi, hususan katika taasisi za elimu ya juu kupitia programu mbalimbali kama vile ***Samia Scholarship Awards***.

Nimefurahishwa pia na ushirikiano kati ya Taasisi ya Benjamin Mkapa na Wizara ya Afya katika kuanzisha jukwaa la vijana kujadili ajenda ya rasilimaliwatu katika sekta ya afya. Suala hili la kimkakati liwe endelevu na lishirikishe vijana wengi kadri iwezekanavyo. Ninawahimiza vijana kutumia

kikamilifu fursa zitokanazo na maendeleo ya teknolojia kama akili unde (*Artificial Intelligence*), tiba kwa njia ya mtandao (*telemedicine*), uchambuzi wa takwimu na teknolojia mpya zitakazoendelea kubadilisha tasnia ya afya.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Mwisho, ningependa kusisitiza ajenda ya Rasilimaliwatu katika Sekta ya Afya (HRH) kuendelea kujengwa na kupewa kipaumbele. Hivyo ninaunga mkono azma ya kuubadilisha Mkutano na Kongamano hili kutoka mkusanyiko wa mara moja kila baada ya miaka miwili, na kuwa jukwaa kuu la Afrika la fikra za kitaalamu, majadiliano ya sera, ubunifu na kubadilishana maarifa kuhusu nguvu kazi ya afya, litakalofanyika mara moja kila mwaka.

Ninawatakia Mkutano Mkuu mwema na wenye mafanikio.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**